



EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

MAOMBI YA TAARIFA YA KUONYESHA NIA KWA AJILI YA KUFANYA TATHMINI YA MADHARA YA KIJINSIA PAMOJA NA USHIRIKISHAJI UNAOJALI JINSIA KATIKA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP) KUMBUKUMBU NA: 0010006758

TOTAL East Africa Midstream B.V (Kampuni) Tanzania, Kampuni ya Mafuta na Gesi, inaalika makampuni yenye uzoefu na sifa kuonyesha nia kwa ajili ya kufanya Tathmini ya Madhara ya Kijinsia pamoja na Ushirikishaji Unaojali Jinsia katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini la kusafirisha Mafuta linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha Mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania na kilomita 296 zitakuwa nchini Uganda. Eneo la bomba katika upande wa Tanzania litapita katika Mikoa nane (8), ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga. Bomba litapita katika Mamlaka za Halmashauri za Wilaya 27 na Vijiji 231. Nchini Uganda, bomba litapita katika wilaya 10 ambazo ni Hoima, Kikuube, Kakumiro, Kyankwanzi, Mubende, Gomba, Sembabule, Lwenga, Rakai na Kyotera ikiwemo Wilaya 27 na vijiji 171.

MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:

KAMPUNI imefanya tafiti tofauti ikiwemo Tathmini ya Athari za Kimazingira na Kijamii, Tathmini ya Athari za Haki za Binadamu na pia kuandaa Mipango Kazi Kumi (10) ya Uhamishaji wa Watu na Makazi kama inavyotakiwa katika Viwango wa Uwezeshaji wa Kifedha vya Kimataifa.

Kwasasa KAMPUNI inahitaji la kufanya Tathmini ya Madhara ya Kijinsia pamoja na Ushirikishaji Unaojali Jinsia kwa ajili ya Mradi ili kuwezesha Mradi kuelewa vyema asili ya madhara yanayohusiana na jinsia yanayoweza kutokea kutokana na Mradi na kubaini njia sahihi za kupunguza madhara hayo na pia kubaini fursa zitakazo leta matokeo chanya kwa wanaume na wanawake katika jamii zinazoguswa na Mradi.

KAMPUNI inahitaji huduma za mashirika ya K Tanzania yenye sifa, uzoefu na yanainazoweza kufanya tathmini kama hii aidha nchini Uganda au Tanzania au katika nchi zote mbili. Shirika linatakiwa kuwa na rekodi ya kufanya uchambuzi wa maswala yaliyojikita kwenye jinsia na kuwa na mtandao hai wa jumua au mashirika ya wanawake katika kila nchi ambayo yanaweza kuchangia maoni kwenye tathmini au kutoa mapendekezo.

Tathmini itajumuisha hatua ya utafiti kwa njia ya computer; hatua ya kukusanya taarifa na kuzifanyia tathmini, kubainisha namna ya kupunguza madhara na njia za kuboresha; na uandaaji wa rasimu ya mpango mkakati wa Jinsia. Tathmini hii itahitaji uwepo wa timu ya USHAURI itakayochaguliwa katika eneo husika/la uwanda.

VIGEZO MUHIMU:

Makampuni/Mashirika yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa usajili wa kampuni au shirika nchini Uganda na/au Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili katika Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) na/ au Uganda (URA) na Cheti cha Ithibati ya Malipo ya Kodi cha mwaka wa hivi karibuni.
- Maelezo kwa ufupi ya uzoefu wa kufanya tafiti za maswala ya kijamii haswa katika mlengo wa uchambuzi wa maswala ya jinsia, tathmini ya athari za kijinsia na uzoefu katika uwanda wa ushiriki unaojali jinsia pamoja na mabadiliko yanayolenga kuleta fursa kwa jinsia zote.
- Maelezo kwa kifupi ya sifa na uzoefu wa watendaji wakuu watakaofanya tathmini katika kila nchi.

Kutokana na asili ya tathmini, Mradi unaalika makampuni yenye sifa au mashirika kuwasilisha taarifa za kuonyesha nia kwa ajili ya tathmini ya Uganda tu, ya Tanzania tu au kwa nchi zote mbili.

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe:

talal.mufti@external.total.com nakala kwa **mihye.allaire@external.total.com** (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa 11:00 jioni Majira ya Afrika Mashariki, tarehe 21st May, 2021.

Muhimu: Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).Language.